MAANDALIZI YA HALI YA HATARI:

Dharura za Wazazi na Shule



Usalama na ulinzi wa wanafunzi na wafanyakazi wetu ni vipaumbele vya juu kwa Shule za Umma za Richmond.

rvaschools.net

RPS
RICHMOND
PUBLIC SCHOOLS

Yaliyomo

Maandalizi ya Hali ya Hatari: Dharura za Wazazi na Shule

3 | Utangulizi

3 | Dharura Ni Nini?

Maandalizi

4 | Wazazi Wanapaswa Kufanya Nini Ili Kujitayarisha Kwa Ajili ya Dharura?

5 | Shule Zitafanya Nini Katika Tukio La Dharura?

6 | Vitendo vya Kinga ambavyo Shule Inaweza Kutumia

8 | Wazazi Wanapaswa Kufanya Nini Katika Tukio la Dharura?

Mawasiliano ya Dharura

10 | Wazazi Wataarifiwaje Tukio Likitokea Shuleni?

10 | Ahueni Baada ya Hali ya Hatari

11 | Kwa Maelezo ya Ziada

11 | Kadi ya Mawasiliano ya Dharura ya Mzazi

MAANDALIZI YA HALI YA HATARI:
DHARURA ZA WAZAZI NA SHULE

Utangulizi

Usalama na ulinzi wa wanafunzi na wafanyakazi wetu ni vipaumbele vya juu kwa Shule za Umma za Richmond (RPS). Kijitabu hiki kinaeleza baadhi ya taratibu ambazo zimepangwa na kutekelezwa katika tukio la dharura shuleni kwa mtoto wako.

Wasimamizi wa shule hufanya kazi kwa karibu na polisi, zimamoto, huduma za dharura na mashirika ya afya ya umma ili kuhakikisha utendakazi ufaao na kwamba shule zote zimeandaliwa kwa ajili ya dharura. Wafanyakazi wakuu wamefunzwa katika taratibu za Mfumo wa Kitaifa wa Kudhibiti Matukio. Tumejitayarisha kufanya kazi kwa ushirikiano na watoa huduma za dharura iwapo kisa kibaya kitatokea katika mojawapo ya shule zetu.

Mpango wetu wa kina wa dharura unashughulikia aina nyingi za matukio yanayoweza kutokea, sio kwa sababu tunatarajia yatokee, lakini kwa sababu tunataka kujiandaa iwapo yatatokea. Kwa sababu za kiusalama, huenda maelezo mahususi yasiweze kupatikana kwa umma; hata hivyo, wazazi na wanafunzi wana jukumu muhimu na ni muhimu ujue unachopaswa kufanya katika dharura. Tafadhali kagua maelezo yaliyo katika kijitabu hiki ili kuhakikisha wewe na mtoto wako mnaelewa taratibu za dharura.

Dharura Ni Nini?

Dharura ni tukio lolote lisilotarajiwa ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa wanafunzi au wafanyakazi. Inaweza kuhusu chochote kutoka kwa usumbufu wa huduma hadi shughuli ya kigaidi na inaweza kuathiri mtoto mmoja, shule moja au wilaya nzima ya shule. Maafisa wa shule, na wakati mwingine wahudumu wa dharura, watatathmini uzito wa kila hali na kubainisha hatua bora ya kujibu haraka, kwa usalama na ipasavyo. Kupanga mapema na maandalizi ya hali ya juu kunaweza kupunguza hatari katika hali yoyote ya dharura. Nyenzo hizi hutoa miongozo ya kujitayarisha, kile ambacho wazazi wanapaswa kufanya, na kile ambacho shule itafanya iwapo dharura itatokea. Taratibu za mawasiliano na taratibu za kuwaruhusu wanafunzi pia zimeainishwa.

MAANDALIZI

Wazazi Wanapaswa Kufanya Nini Ili Kujitayarisha Kwa Ajili ya Dharura?

Wazazi wana jukumu muhimu la kuwatayarisha watoto wao kwa ajili ya dharura. Yaliyoorodheshwa hapa chini ni baadhi ya njia unazoweza kuwasaidia kuelewa kwamba dharura ikitokea shuleni, walimu na maafisa wa shule hufunzwa kushughulikia hali hiyo. Wahakikishie kuwa utawasiliana na shule na utaungana tena nao mara tu ikiwa salama kufanya hivyo.

- Hakikisha maelezo ya mawasiliano ya dharura yamesasishwa na ni sahihi. Wasiliana na afisi ya mapokezi ya shule mara moja wakati umebadilisha anwani yako au nambari ya kazini, nyumbani au ya mkononi.

- Mjulishe muuguzi wa shule kuhusu hali zozote za kiafya au vizuizi vya kiafya ambavyo mtoto wako anaweza kuwa navyo au dawa ambazo mtoto wako anaweza kuwa anatumia. Toa vifaa vya matibabu na dawa zinazohitajika kwa ajili ya matumizi ya kila siku na ugavi wa ziada wa mtoto wako kuleta shuleni wakati wa dharura. Ikiwa kuna maswali kuhusu kiasi kinachofaa cha dawa au vifaa, tafadhali wasiliana na mtoa huduma wa matibabu wa mtoto wako.

- Tambulisha ni nani aliyeidhinishwa kumchukua mtoto wako ikiwa hutaweza kufikiwa. Hakikisha kuwa maelezo yao ya mawasiliano yamesasishwa na sahihi, na yapo kwenye faili shuleni. Tafadhali elewa kwamba mtoto wako ataruhusiwa kwenda na wazazi na watu waliotambuliwa kwenye orodha ya mawasiliano ya dharura pekee. Jadili kuhusu maelezo haya na mtoto wako.

- Hakikisha mtoto wako anajua jina la mzazi au mlezi, anwani na nambari za simu za mzazi wake. Iwapo kuna mzazi au mlezi mmoja tu, mtoto wako anapaswa kuwa na maelezo ya mawasiliano ya mtu mzima wa pili anayewajibika.

- Zungumza na mtoto wako kuhusu umuhimu wa kuwa mtulivu na kufuata maelekezo iwapo kutakuwa na dharura. Dharura ikitokea wakiwa shuleni, mwalimu wao atawapa maagizo na maelezo yanayofaa.

- Mjulishe mtoto wako kwamba anaweza kuhamishwa hadi mahali pengine hadi uweze kumchukua. Eleza neno “uhamisho” ili wasiogope kuhamishwa kutoka shuleni kwao. Ufafanuzi rahisi wa uhamisho ni mchakato wa kuwahamisha watu mbali na eneo ambalo wako hatarini na kuwapeleka mahali salama.

- Mueleze kwamba simu za mkononi hazipaswi kutumiwa wakati wa dharura isipokuwa kama ameagizwa kufanya hivyo na mwalimu. Wahudumu wa dharura watategemea simu za mkononi kwa mawasiliano. Iwapo wanafunzi na wazazi wanajaribu kuwasiliana, saketi za simu za mkononi zinaweza kuzidiwa, hivyo kutatiza uwezo wa wafanyakazi wa dharura kuwasiliana taarifa muhimu.

- Wakati wowote upo kwenye mazingira ya shule, endeleo kuwa chonjo ili uone shughuli za ndani na nje ya shule. Ripoti shughuli zozote za kuleta shaka kwa wasimamizi wa shule ili waweze kuchunguza.

- Anzisha mpango wa maandalizi ya familia ikijumuisha mpango wa mawasiliano. Hii itakuwezesha kuwasiliana na wanafamilia wote wakati kuna hali ya dharura.

- Iwapo kuna hali ya dharura ambapo mtoto wako hawezi kwenda nyumbani kwao, hakikisha kuna mahali pengine anapoweza kwenda na pawe salama huku akisubiri mwanafamilia aje awachukue.

Shule Zitafanya Nini Katika Tukio La Dharura?

Tunachofanya wakati wa dharura hutegemea hali na maelezo mahususi ya tukio. Tutajitahidi tuwezavyo kuhakikisha kwamba mafundisho yanaendelea, hata tunapolazimika kufunga shule. Kulingana na ukubwa wa tishio au dharura, hatua za ziada zinaweza kuchukuliwa, ikiwemo kuwahifadhi mahali salama, kuwahamisha wanafunzi kutoka kwenye majengo au kufunga shule mapema.

Iwapo wahudumu wa dharura wataitwa kwenye eneo la tukio, tutashirikiana nao kwa amri ya pamoja ili kubainisha ni mpango ambao unapaswa kutekelezwa. Mipango ya dharura ya shule hutofautiana kulingana na shule, kulingana na saizi ya shule, mpangilio wa jengo na mambo mengine muhimu, na huanzishwa kulingana na matukio yanayotokea wakati wa tukio. Ingawa kila shule imeweka mipango ya utekelezaji, maeneo ya uhamishaji na mipango ya kuungana na familia, ni lazima mipango hii iendelee kuwa rahisi kutekelezeka kadiri hali inavyobadilika. Wazazi watajulishwa punde tutakapofanya kila tuwezalo ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi na inapowezekana kutoa taarifa sahihi na muhimu.

Vitendo vya Kinga ambavyo Shule Inaweza Kutumia

Kila shule ina mpango wa maandalizi ya dharura unaohusisha hatua kadhaa zinazowezekana. Majibu hutofautiana, kulingana na hali, na huamuliwa na timu iliyofuzu ya kukabaliana na hali ya hatari kufanya maamuzi kama haya. Ni muhimu kwa wazazi kuelewa kwamba ikiwa tukio yenye hatari litatokea, wanafunzi wataruhusiwa kwenda kwa wazazi ikiwa hatari imekwisha. Shule zinaweza kutumia hatua zifuatazo za kinga:

- **Kufungwa.** Shule inaweza kufungwa kwa sababu kuna tukio ndani ya majengo au kwa sababu kuna kitu kinatokea nje na polisi wameona ni vyema kuhakikisha kuwa shule inalindwa. Madhumuni ya kufunga shule ni kuzuia harakati za wafanyakazi na wanafunzi, na kulinda majengo kabisa.

  Wakati shule umefungwa, milango yote ya ndani na nje hufungwa. Hakuna mtu anayeruhusiwa kuingia au kutoka ndani ya majengo hayo hadi maafisa wa shule, mara nyingi wakifanya kazi kwa kushirikiana na polisi, wathibitishe kuwa ni salama kufanya hivyo. Wafanyakazi, wanafunzi na wageni wote watahesabiwa na mafundisho yataendelea. Urefu wa kipindi cha shule kufungwa unategemea hali maalum, na unaweza kuwa dakika chache au saa kadhaa. Inawezekana kuwa shule kufungwa kunaweza kuhusisha kuwazuia wanafunzi kuwa muda zaidi ya siku ya kawaida ya shule. Sio nia yetu kamwe kuwazuia wanafunzi isivyohitajika, na hatutafanya hivyo isipokuwa ili kuhakikisha usalama wao.

  Hali zitarejea kuwa ya kawaida punde tu kunapokuwa salama kufanya hivyo. Wazazi wanaweza kujulishwa au wasijulishwe wakati shule imefungwa. Kuna nyakati ambapo shule hufungwa kwa ajili ya mazoezi au mafunzo, au kwa tukio la nje ambalo halihusishi shule. Msimamizi wa shule na Mkurugenzi wa Ulinzi na Usalama watabainisha wakati tukio ni muhimu kiasi cha kuwajulisha wazazi.

- **Mahali salama.** Kitendo hiki cha ulinzi huzingatiwa tukio linapofanyika nje ya shule na maafisa wameamua kwamba hatua salama zaidi ni kuwaweka wanafunzi na wafanyakazi ndani ya shule hadi tukio la nje litakaposhughulikiwa. Baadhi ya mifano inaweza kuwa kwa sababu ya hali ya hewa, utoaji wa nyenzo hatari, au hali inayotokea katika jamii ambapo watoto hawapaswi kuruhusiwa kwenda. Wanafunzi walio nje watarudishwa ndani, wakiwemo wanafunzi walio katika madarasa ya nje au trela. Ikiwa mahali salama itahitajika na inaweza kutumika zaidi ya saa za kawaida za siku ya shule, wazazi watajilishwa kwa haraka iwezekanavyo.

- **Uhamisho.** Iwapo sio salama kwa wanafunzi na wafanyakazi kubaki ndani ya majengo hayo, shule itahamishwa. Wanafunzi na wafanyakazi wanaweza kubaki kwenye uwanja wa shule hadi majengo yatakapokuwa salama kuingia tena au kuhamishwa hadi mahali salama nje ya mali ya shule, kulingana na hali mbalimbali. Katika tukio la kuhamishwa nje ya chuo, wasimamizi wa shule watashirikiana na maafisa wa dharura na Idara ya Uchukuzi ili kuwahamisha wanafunzi kwenda mahali salama. Kutoka hapo wanafunzi watasafirishwa kwenda nyumbani au kusubiri wanafamilia kuwachukua kutoka kwenye kituo cha kuungana na familia. Katika tukio lolote lile, msimamizi wa shule na Mkurugenzi wa Mawasiliano watahakikisha kwamba wazazi wamearifiwa.

- **Shule Kufungwa Dharura.** Utaratibu huu utafanyika wakati wasimamizi wa shule watabaini kuwa wanafunzi wako salama nyumbani kuliko shuleni. Mara nyingi hii hutokea kwa sababu ya huduma kupotea au dharura ya hali ya hewa. Wazazi wataarifiwa kwamba shule zitafungwa. Katika hali ya kawaida, wanafunzi ambao kwa kawaida hupanda basi watasafirishwa hadi nyumbani na wazazi wataarifiwa.

- **Kuungana na Familia Nje ya Kituo.** Wanafunzi huhamishwa nje ya kituo wakati maafisa wa shule wameamua kwamba wanafunzi na wafanyakazi hawafai kuingia tena ndani ya majengo hadi itakapokuwa salama. Maeneo kadhaa ya nje ya kituo huamuliwa mapema, lakini hayashirikiwi na wazazi hadi tukio litakapotokea. Polisi na maafisa wa shule huchagua kituo bora ya kuungana tena na familia wakati wa tukio kulingana na hali ya dharura. Wazazi wataarifiwa kuhusu kituo cha kuungana na familia punde itakapofaa kufanya hivyo. Vipaumbele vyetu vikuu katika uhamisho wa nje ya kituo ni usalama wa wanafunzi na uwajibikaji. Tunataka kuhakikisha kuwa wanafunzi wameruhusiwa kwenda kwa watu binafsi walioidhinishwa na utaratibu wa kutoka utaanzishwa.

Katika tukio la kuhamishwa kwenye kituo kilicho nje ya shule, wazazi watapewa maelezo kuhusu mahali ambapo kituo cha kuungana tena kinapatikana. Wazazi au watu wazima walioidhinishwa watahitajika kuonyesha kitambulisho cha picha ili kumchukua mtoto. Huenda mchakato ukachukua muda kwa sababu tunataka kuhakikisha kuungana tena na familia kunafanywa na watu walioidhinishwa.

Wazazi Wanapaswa Kufanya Nini Katika Tukio la Dharura?

Majibu yenye manufaa zaidi ya wazazi wakati wa dharura ya shule ni kuwa mtulivu na kusubiri taarifa sahihi kutumwa kwa nambari iliyoorodheshwa kwenye anwani ya dharura ya mtoto wako kwa kutumia **Mfumo wa Remind wa Utumaji Ujumbe** (www.rvaschools.net/remind). Tunaelewa kuwa ni jambo la kawaida kwa wazazi kutaka kumkimbilia mtoto wao. Ni muhimu uelewe kwamba, wakati wa tukio kama hilo, shule binafsi na wahudumu wa dharura wamejiandaa kushughulikia matukio haya. Ushirikiano wako katika hali ya dharura ni muhimu kwa utatuzi salama na wa haraka wa tukio.

- Tafadhali usipige simu shuleni. Ni muhimu kuendelea kufungua simu ili viongozi wa shule waweze kupiga simu za dharura. Ikiwa wanafunzi ni wagonjwa au wamejeruhiwa, wazazi wa wanafunzi hao wataarifiwa kwanza.

- Tafadhali usiende shuleni. Kama tulivyojifunza kutokana na dharura za awali shuleni, mojawapo ya changamoto zetu kuu ni jinsi ya kudhibiti umati wa wazazi na wananchi wanaojali wanaokimbilia kwenye eneo la tukio “kusaidia.” Kwa kufanya hivyo, wazazi wanaweza kuanzisha msongamano wa magari bila kukusudia ambao unaweza kuwazuia wahudumu wa dharura kufika kuondoka kwenye eneo la tukio, ikihitajika, kuwasafirisha wafanyakazi au wanafunzi waliojeruhiwa hadi kwenye vituo vya matibabu ya dharura.

- Endelea kuwa mtulivu, kufuata taratibu na kushirikiana na maafisa wa shule na usalama wa umma.

- Endelea kuwa karibu na simu iliyoorodheshwa kama nambari yako ya mawasiliano ya dharura.

- Pata taarifa za hivi punde kuhusu tukio hilo kutoka kwa tovuti ya wilaya katika **www.rvaschools.net**.

MAANDALIZI

- Fahamu kuwa taratibu za dharura za kuchukua ni tofauti na taratibu za kawaida za kuchukua. Iwapo utaarifiwa umchukue mtoto wako shuleni au katika kituo kilichoteuliwa cha kuungana na familia, leta kadi ya kitambulisho cha picha. Iwapo ni lazima utume mtu mwingine kuchukua mtoto wako, hakikisha kuwa ni mtu ambaye ameorodheshwa kwenye rekodi za shule kama mtu aliyeidhinishwa na anamiliki kitambulisho cha picha. Mtoto wako hataruhusiwa kwenda kwa mtu yeyote ambaye hajaidhinishwa au ambaye hawezi kutoa kitambulisho kinachofaa.

- Fuata taratibu za dharura. Ukiombwa umchukue mtoto wako, utaombwa ufuate utaratibu wa kumchukua uliowekwa kwa ajili ya dharura. Mfumo wa kuungana na familia uliundwa ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi wote na ni muhimu kufuata utaratibu huo.

- Salia kwenye maeneo yaliyoteuliwa kwenye kituo cha kuungana na familia.

- Kuwa mtulivu. Ni muhimu kwamba utaratibu wa kuungana na familia utatekelezwa kwa utaratibu ili tuweze kuwalinda na kuwajibika kwa ajili ya wanafunzi wetu wote.

MAWASILIANO YA DHARURA

Wazazi Wataarifiwaje Tukio Likitokea Shuleni?

Kipaumbele chetu cha kwanza ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wako salama, tunawajibika kwa ajili yao, na wako chini ya uangalizi wa watu wazima. Mara tu inapowezekana kufanya hivyo, Mkurugenzi wa Mawasiliano atawasilisha taarifa kwa wazazi na jamii. Wilaya ya shule ina aina mbalimbali za vyombo vya habari vinavyopatikana kwa wazazi ambavyo vitasasishwa, inapohitajika, na taarifa kamili na sahihi zinazopatikana.

1. Tovuti ya RPS (www.rvaschools.net)
2. Arifa za Ujumbe za Remind (mawasiliano ya moja kwa moja ya simu za mkononi katika kiwango cha shule)

Katika tukio la dharura kubwa, wazazi wanahimizwa kutazama mojawapo ya vituo vifuatavyo vya televisheni vya ndani kama chanzo cha ziada cha kupata habari:

- Kituo cha 6 – CBS
- Kituo cha 8 – ABC
- Kituo cha 12 – NBC

Tafadhali kumbuka kuwa ingawa vituo vya televisheni vinalenga kuripoti taarifa za sasa, hatuwezi kuhakikisha kuwa vinaripoti taarifa zote kwa usahihi, na wazazi/walezi wanapaswa kuangalia kwanza mifumo rasmi ya RPS iliyobainishwa hapa juu.

Ahueni Baada ya Hali ya Hatari

Maafisa wa shule wanaelewa kwamba tukio hatari shuleni au katika jumuiya linaweza kuwa na athari ya kihisia kwa wafanyakazi na wanafunzi. RPS ina timu iliyofunzwa ya washauri, wahudumu wa jamii, na wanasaikolojia ambao wanaweza kujibu shule wakati na baada ya tukio hatari ili kutoa usaidizi. Iwapo tukio hatari linaweza kuwa na athari ya kihisia kwa wafanyakazi au wanafunzi, timu ya misaada RPS huwasaidia walioathirika kukabiliana na matokeo ya tukio hilo.

MAWASILIANO YA DHARURA

Kwa Taarifa ya Ziada

- Kwa taarifa ya ziada kuhusu Mpango wa Usalama na Hali ya Hatari ya RPS, wasiliana na Monica Fecht katika mfecht@rvaschools.net.
- Tembelea www.rvaschools.net/schools-office/safety-and-security
- Kwa taarifa kuhusu Mpango wa Usalama na Hali za Hatari za shule ya mtoto wako, wasiliana na msimamizi wa shule.
- Rejelea tovuti hii kwa rasilimali za maandalizi ya dharura: www.ready.gov.

Kadi ya Mawasiliano ya Dharura ya Mzazi

Kwa manufaa yako. Tafadhali chapisha na ukunje kadi ya pochi ili itumike katika hali ya dharura.



RPS

RICHMOND

PUBLIC SCHOOLS

rvaschools.net